JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI


Simu Na: +255 (026) 2963309/13/14
Nukushi: +255 (026) 2963316
Barua Pepe: ps@lands.go.tz
Tovuti: www.lands.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
2 Mtaa wa Ardhi,
S.L.P. 2908,
**40477 DODOMA**.


## TAARIFA KWA UMMA
## KUH: KISIWA CHA LUPITA KILICHOPO KATIKA ZIWA TANGANYIKA, TANZANIA

**Dodoma 31 Agosti 2026**

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeona kupitia mitandao ya kijamii taarifa kuwa mwekezaji Bw. Tim Draper anakusudia kuuza ardhi katika kisiwa kilichopo Ziwa Tanganyika nchini Tanzania.

Wizara inapenda kuutaarifu umma kuwa, kisiwa kinachorejewa kinafahamika kama Kisiwa cha Lupita kilichopo katika Ziwa Tanganyika Wilaya ya Nkasi Mkoa wa Rukwa. Kisiwa hiki ni moja ya maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji chini ya Mamlaka ya Uwekezaji na Usimamizi wa Maeneo ya Uwekezaji (TISEZA) na kimepangishwa kwa kampuni ya Firelight Safaris Ltd ambayo Bw. Tim Draper (Raia wa Marekani) ni miongoni wa wanahisa.

Sheria ya Ardhi Sura ya 113 imeweka utaratibu wa namna wawekezaji raia wa kigeni wanavyoweza kupata ardhi kwa ajili ya uwekezaji chini ya Mamlaka ya Uwekezaji na Usimamizi wa Maeneo ya Uwekezaji (TISEZA). TISEZA ambao ndio wamiliki kwa mujibu wa sheria, wamepangisha eneo hilo na kutoa Hakimiliki Isiyo ya Asili (Derivative Right) kwa kampuni ya Firelight Safaris Ltd kwa matumizi ya hoteli ya kitalii.

Hivyo kampuni ya Firelight Safaris Ltd ni mwekezaji halali katika eneo hilo na anaweza kuhamisha uwekezaji wake kwenda kwa mwekezaji mwingine kwa kuzingatia sheria na taratibu za Nchi.

Imetolewa na

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**